



No. 3 G Chabruma Street off Ali Hassan Mwinyi Rd,
Ada Estate, Mbuyuni, Kinondoni Dar es Salaam
P.O. Box 60243, Dar es Salaam TANZANIA

+255-22-2666441

+255-766-430337/655-730337

Email: mariaclinic@ymail.com

Website: www.hmmcltd.com

HEALTH PUBLICATIONS / MAKALA YA AFYA

KUKUA KWA MATITI KWA MWANAUME (GYNAECOMASTIA)

Kwa kawaida kukua kwa matiti husababishwa na homoni za kike wakati homoni za kiume huzuia ukuaji wa matiti na hivyo ni lazima kuwe na uwiano sahihi kwa upande wa mwanamke (kuwa na homoni za kike nyingi na za kiume kidogo) na kwa mwanaume (kuwa na homoni za kiume nyingi na za kike chache) ili matiti yakue kwa mwanamke na yasikue kwa mwanaume. Uwiano huu unapopata hitilafu kwa upande wa mwanaume, matiti yanaweza kukua.

Matiti yanaweza kuwa makubwa kidogo kuzunguka chuchu au yanaweza kuwa makubwa kiasi cha kuchukua sura ya matiti ya mwanamke; inaweza kutokea kwenye titi moja au yote mawili; na yanaweza kuambatana na maumivu au bila maumivu. Kukua kwa matiti kwa mwanaume kunaweza kukawa kwa sababu ya mabadiliko ya homoni ya mwilini au inaweza kuletwa na magonjwa.

Kuna vipindi vitatu vya ukuaji ambavyo kunaweza kutokea mabadiliko ya homoni ambayo yanasababisha ukuaji wa matiti kwa watu wa jinsia ya kiume. Kipindi cha kwanza ni wakati wa mtoto akiwa mchanga, cha pili ni wakati ya kubalehe na cha tatu ni uzeeni. Mtoto anapozaliwa anakuwa na homoni za mama nyingi na wakati mwingine zinaweza kusababisha matiti ya mtoto kuwa makubwa kiasi. Hali hii hupotea baada ya wiki chache. Kipindi cha kubalehe matiti yanaweza kukua kwa sababu ya kuchelewa kwa kuongezeka kwa homoni za kiume ambako kunatakiwa kutokea katika kipindi hiki. Hii ni sababu mojawapo kubwa ya tatizo la matiti kukua kwa mwanaume na hali hii hopetea katika kipindi cha mwaka mmoja au miwili. Wakati wa uzeeni homoni za kiume hupungua kiwango na hivyo inaweza kusababisha matiti kukua.

Sababu nyingine za kukua kwa matiti kwa mwanaume ni dawa za kutibu baadhi ya magonjwa; baadhi ya madawa ya kulevya; kunywa pombe kupita kiasi; magonjwa kama vile ya figo na ini; magonjwa ya kurithi yanayoathiri korodani; na baadhi ya vivimbe vinavyotoa homoni za kike kwa wingi.

Matibabu yatategemea na kipindi cha ukuaji ambapo tatizo limetokea na kama kuna sababu maalumu kwa (mfano uvimbe) ambao umesababisha mabadiliko ya homoni. Hivyo basi wataalamu wa afya watashauri njia inayofaa.

Na Madaktari bingwa wa magonjwa ya Homoni na Uzazi – Maria Clinic

Kwa Huduma ya Kuonana na Daktari Bingwa piga simu namba:

+255 766 430 337/+255 754 587900/+255 755 085586